**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE**

**SHULE YA SEKONDARI YA UFUNDI SONGWE**
**S.L.P 77**
**MKWAJUNI-SONGWE**
**27/11/2025**

**MAWASILIANO**
**MKUU WA SHULE 0655753012/ 0766723012**
**MWALIMU PERSIS PATRICK MWAVEYAH 0745749003**
**MWALIMU PRISCA DAMAS MUSHI 0754370144**
**Kumb.Na.STS.E/F1/2025**

MZAZI/MLEZI WA…………………………………………………………………………………………………
S.L.P……………………………………………………………………………………………………………….
…………………………………………………………………………………………………………………….

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI YA AMALI SONGWE ILIYOPO HALMASHAURI YA SONGWE MKOA WA SONGWE JANUARY 2026(JOINING INSTRUCTION)**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga katika shule hii katika mwaka wa masomo 2026. Shule hii ni ya bweni na ni mchanganyiko wa wavulana na wasichana.

Shule ya Ufundi –Songwe iko umbali wa Km 82 kutoka Mji Mdogo wa Mbalizi na Km 8 kutoka Mkwajuni. Usafiri kutoka Mbalizi upo muda wote nauli ni Shilingi 8,000 na kutoka Mkwajuni nauli ni Shilingi 2,000 unashukia Iseche Songwe sekondari.

Wewe ni miongoni mwa wanafunzi wachache waliobahatika kuchaguliwa kuendelea na masomo ya sekondari hivyo unatakiwa kuwajibika kikamilifu katika kutekeleza maagizo yote kwa busara, hekima, utii na uaminifu.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 13/01/2026, Hivyo mwanao anatakiwa kufika shuleni tarehe 10/01/2026 kabla ya saa kumi na mbili jioni.

2. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**A. SARE YA SHULE**

Mzazi anatakiwa kumnunulia mwanae sare ya shule kama ifuatavyo:-

**a. WASICHANA**

i. Sketi mbili (2) za rangi ya KAKI (Grade one) inayofanana kama ya polisi. Sketi ziwe na marinda 16 nane kila upande yaliyopangwa kuelekea kulia na ziwe ndefu zinazofika kwenye vifundo vya miguu.
ii. Shati mbili (2) nyeupe aina ya tomato za mikono mifupi.
iii. Tai ya rangi nyeusi iwe spesho.

Kwa wanafunzi wasichana wa kiislamu wanapaswa kuwa na

iv. Ushungi mbili nyeupe ziwe pana ndefu zinazofunika kifua.Ushungi hazipaswi kufunika viganja vya mikono,zisifunike uso pia zisiwe nyepesi na wala zisiwe na urembo wowote.
v. Blauzi(Nusu kanzu) mbili (2) nyeupe za mikono mirefu zisizofunika viganja vya mikono ,ziwe pana isibane, pia iwe ndefu inayoishia juu ya magoti,isiwe kama gauni na isiwe nyepesi.
vi. Viatu vya shule vyeusi vya ngozi jozi 2.viwe vya heshima vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba
vii. Soksi rangi nyeupe.
viii. Vifaa vya michezo raba,viatu vya michezo bukta rangi ya kijani,stokings(soksi ndefu) jozi mbili
ix. Tracksuit moja rangi nyekundu zenye ufito mweupe
x. Shuka rangi ya pink jozi mbili
xi. Gauni mbili (shamba dress ya rangi ya light blue kwa ajili ya kushindia. Mshono ni solo ndefu

**b. WAVULANA**

i. Suruali (2) mbili rangi ya kaki inayofanana kama ya polisi(grade one) ya heshima siyo modo iwe na marinda mawili
ii. Mashati mawili rangi nyeupe mikono mifupi aina ya tomato yote yawe marefu yakuweza kuchomekea kwenye suruali
iii. Tai nyeusi ndefu spesho
iv. Viatu vya shule vyeusi vya ngozi jozi 2 viwe vya heshima vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba.
v. Soksi rangi nyeusi angalau jozi tatu
vi. Mkanda mweusi wa suruali usio na picha wala madoido
vii. Vifaa vya michezo raba/viatu vya michezo bukta rangi ya blue, stokings (soksi) ndefu jozi mbili
viii. Tracksuit moja rangi ya blue iliyokolea yenye ufito mweupe.
ix. Shuka rangi ya blue jozi mbili

x. Shamba dress suruali ya kijivu na tisheti rangi ya maruni ambayo itapatikana shule kwa shilingi 15000/=.

**3. MAHITAJI YA PAMOJA**

1. Madaftari 18 makubwa counter (Quire 2 au zaidi)
2. Begi la kubebea madaftari (school bag) lisiwe la nailon au plastic wala lisiwe na maandishi makubwa au picha
3. Kompasi (Mathematical set)
4. Kalamu, penseli, rula, vifutio vya kutosha
5. Kamusi (English/Swahili au English/English) kila mwanafunzi anatakiwa aje na ya kwake
6. Rim 1 ya karatasi nyeupe A4 kwa ajili ya kuchapishia mitihani na rim ya A3 kwa ajili ya michoro
7. Ufagio wa chelewa
8. Sabuni kwa ajili ya vyooni aina ya ARO ya lita moja kwa wote
9. Jembe 1 lenye mpini wavulana wote
10. Soft blooms –wasichana wote
11. Hard blooms-wavulana wote
12. Ovaroli 01 rangi ya darkblue
13. Kwanja wasichana wote
14. Sweta rangi ya maruni
15. .Saa ya mkononi kwa ajili ya kutunza muda
16. Chandarua rangi ya blue
17. Godoro la sponji ukubwa wa 2.5x6
18. Kikokotoo(calculator) casio yenye f(x)991,safety boots,kofia ngumu,Dust musk
19. Mto na foronya inayofanana na rangi za shuka yako
20. Blanket moja
21. container dogo la kulia chakula,kikombe na kijiko
22. Ndoo ndogo ya kuogea na kufulia
23. Sanduku la bati kwa ajili ya kuhifadhia vitu
24. Taulo maalumu kwa watoto wa kike{pedi } angalau bunda 2
25. Nguo za ndani za kutosha
    A. Wasichana taiti kuanzia 3, chupi kuanzia 6, kanga au kitenge doti moja
    B. Wavulana boxer angalau 6 , Taulo
26. Picha 2 za passportsize za hivi karibuni.

**VIAMBATISHO VYA KUREJESHA SHULENI**

Mwanafunzi anatakiwa akamilishe/ ajaze fomu zifuatavyo ambazo baadhi zimeambatanishwa

I. Fomu ya kupimwa afya (medical examination form) iwe imejazwa na daktari wa ngazi ya wilaya au zaidi iwe hospitali ya serikali
II. Kopi ya cheti cha kuzaliwa na file rangi ya bluu kwa kuhifadhia nyaraka zake
III. Fomu ya taarifa binafsi ijazwe na mzazi/mlezi
IV. Fomu ya kukubali kutii sharia za shule "Mwanafunzi ahakikishe amezisoma makini na kuzielewa akiwa na mzazi /mlezi wake
V. Fomu yenye majina, namba za simu na picha ndogo 4 za wazazi/ndugu/jamaa wa karibu wanaoweza kumtembelea au kuitwa shuleni panapotokea tatizo ziwe zimebandikwa
VI. Uje na joining instruction ikiwa imejazwa na kurasa zote

**BIMA YA AFYA**

Kila mwanafunzi aje na bima ya afya yenye uwezo wa kupata huduma mahala popote

**MITIHANI**

Kila muhula wanafunzi wanafanya mitihani na matokeo kutumwa kwa wazazi .Mhimize mtoto wako ajitahidi kujisomea na asipate wastani **CHINI YA 55%**

Pia mzazi/mlezi jitahidi kumnunulia vitabu mwanao kulingana na masomo ,vitabu pendekezwa ni vitabu vya TIE.

**MUHIMU**

- Wazazi / walezi na ndugu wengine wanaweza kumtembelea mwanafunzi jumapili ya mwisho wa mwezi kuanzia saa 4 Asubuhi mpaka saa 10 jioni, mgeni yeyote hataruhusiwa kwenda maeneo ya mabweni wala kumletea mwanafunzi chakula.
- Kukiwa na dharura ambayo inamlazimu mzazi/mlezi aje shuleni siku tofauti, dharura hiyo itashughulikiwa na ofisi ya mkuu wa shule
- Endapo itatokea tatizo la msiba mwanafunzi ataruhusiwa kuhudhuria mazishi ya baba mzazi, mama mzazi, kaka au dada wa kuzaliwa pamoja tu.
- Mwanafunzi atapokelewa shuleni akiwa amevaa sare za shule na si vinginevyo, haruhusiwi kuja akiwa amevaa nguo za nyumbani
- Shule hii ni ya serikali haina dini maalumu na inazingatia katiba na sharia za nchi kuhusu uhuru wa kuabudu hivyo wanafunzi wataruhusiwa kufanya ibada kulingana na imani zao.
- Mwanafunzi aje na fedha ya matumizi ambayo itatunzwa na matron wa shule na kupewa kidogo kidogo kwa kusaini kadiri atakavyokua anahitaji. Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na fedha zaidi ya shilingi 5000 bwenini

**KIKAO CHA WAZAZI**

Kutakua na kikao cha wazazi kitakachofanyika 3/10/2025 saa 3 asubuhi lengo la kikao hicho ni kumpa mzazi fursa kuona shule ya mwanaye na kujua mipango na maendeleo ya shule hususani jinsi ya kukuza Taaluma na nidhamu ya wanafunzi

T**AHADHARI**

Tunza fedha zako na vifaa vyako uwapo safarini. Epuka kupokea vyakula kutoka kwa mtu usiyemfahamu pia ni marufuku kumpatia mwanao simu awapo shuleni

**NAKUTAKIA SAFARI NJEMA, KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA AMALI SONGWE**

....................................................................

**S.L.KADINDE**

**MKUU WA SHULE**

**SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE**

Sheria,taratibu na kanuni za shule zimewekwa kwa lengo la kumwezesha mwanafunzi kuelimika na kumaliza elimu yake kwa utulivu na mafanikio makubwa.Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya mwanafunzi atakayevunja sharia,kanuni na taratibu hizo kwa makusudi.Hatua hizo ni pamoja na adhabu ndogondogo shuleni,kusimamishwa shule na au kufukuzwa shule kulingana na uzito wa kosa.Hivyo ni vyema kila mwanafunzi afuate sheria ,kanuni,na taratibu hizo kwa kutumia hekima,akili,bidii,utii na busara na uaminifu ili kuepukana na uvunjifu wa sheria,kanuni na taratibu za shule usiokuwa wa lazima.

1. **HESHIMA, USAFI NA UTUNZAJI WA MALI YA UMMA**

Kila mwanafunzi anatakiwa

i. Kuheshimu walimu na wafanyakazi wote,wanafunzi wenzake na wanajumuiya wote
ii. Kushiriki katika kazi mbalimbali za shule
iii. Kuheshimu ratiba nzima ya shule
iv. Kila mwanafunzi atapangiwa eneo lake la kufanyia usafi kila siku na pia atakua na zamu ya kudeki darasa,bwalo la chakula,vyoo, na bweni lake na atatakiwa kufanya usafi kwa wakati uliopangwa.
v. Kila mwanafunzi atatakiwa kuvaa sare rasmi ya shule wakati wote anapotakiwa na awe tayari kwa ukaguzi wakati wowote.
vi. Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza mali zote zilizopo shuleni.Mwanafunzi atakaye haribu au kupoteza mali ya shule kwa makusudi au uzembe atawajibika kulipia uharibifu au upotevu huo.

**Mwanafufunzi haruhusiwi:-**

a) Kuvuta sigara,bangi wala madawa ya kulevya
b) Kufuga kucha,nywele wala ndevu
c) Kuvaa mavazi yasiyo na heshima kama sketi fupi au suruali ya kubana
d) Kugombana
e) Kutukana au kutoa lugha za matusi kwa mtu yeyote
f) Kunyoa nywele mitindo ya kihuni kwa mfano kipara,panki/kiduku au kusuka
g) Kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa ya mwalimu

h) Kupaka lipstick au kutinda nyusi na kupaka wanja.

2**. MAHUDHURIO**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria

i. Vipindi vyote vya masomo ya darasani na vya nje ya darasa
ii. Miito na mikutano yote kwa mfano Roll calls
iii. Kutunza muda wa ratiba yote ya shule
iv. Kufanya maandalio ya jioni (preparation)
v. Kufanya majaribio na mitihani yote atakayopewa,Akiacha kufanya mtihani /jaribio atahesabiwa kutumia rasilimali za shule vibaya na hivyo atalazimika kulipa **REAM** moja ya karatasi kwa kila mtihani aliokosa bila sababu za msingi.

3. **MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABAISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Uvutaji wa bangi na madawa mengine ya kulevya
iv. Ubakaji na ulawiti
v. Makosa ya jinai
vi. Kupiga au kupigana
vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule
viii. Kudharau Bendera ya Taifa
ix. Kuoa au kuolewa
x. Kumpa mimba msichana/mwanamke
xi. Kutohudhuria vipindi vya masomo bila sababu ya msingi
xii. Kukataa adhabu
xiii. Kunyanyasa wanafunzi wengine
xiv. Kulala nje ya shule bila ruhusa maalumu
xv. Kuanzisha,kuhamasisha,au kushiriki mgomo na vitendo vya uvunjifu wa amani ,fujo,au kufanya maandamano yasiyokuwa halali
xvi. Kumiliki simu ya mkononi ,radio,ipad au camera
xvii. Kupata ujauzito(wasichana watapimwa ujauzito mara kwa mara)
xviii. Kutoa au kushiriki kutoa mimba

B.**MAKOSA MENGINE**

- Hairuhusiwi kwenda kwenye nyumba za walimu /wafanyakazi bila ruhusa
- Hairuhusiwi kutoka nje ya shule bila sare na gate pass
- Hairuhusiwi kuingia katika vilabu vya pombe na baa au night clubs
- Hairuhusiwi kuvaa pete,bangili,hereni,mikufu au kidani
- Hairuhusiwi kumpeleka mgeni yeyote bwenini au kumruhusu kulala bwenini
- Hairuhusiwi kwenda na chakula bwenini
- Hairuhusiwi kwenda na ndala au yeboyebo bwaloni

4. **MABWENI**

Wanafunzi hawaruhusiwi kupika mabwenini au sehemu yeyote ile,kutumia pasi ya umeme mabwenini au kuwa na heater;Pia hawaruhusiwi kuunganisha umeme au kutengeneza unapokuwa na hitilafu.

5. **MATIBABU**

i. Wagonjwa wote wanatakiwa kutibiwa zahanati
ii. Itokeapo dharura ya ugonjwa wakati wa masomo,itamlazimu mwanafunzi kupata kibali cha maandishi cha mwalimu wake ili aweze kutibiwa
iii. Shule haina utaratibu wa kuwapa wanafunzi vyakula maalumu(special or light diet) wazazi/walezi wana jukumu la kuona ni jinsi gani watoto wao wenye mahitaji maalumu ya vyakula watakavyohudumiwa.
iv. Mwanafunzi awe na daftari dogo kwa ajili ya matibabu

**FOMU YA KUKUBALI SHERIA ZA SHULE**

**JINA LA MWANAFUNZI………………………………………………………………………………………………………………………………………….**

**TAREHE YA KUZALIWA…………………………………………………………………………………………………………………………………**

**JINA LA MZAZI/MLEZI…………………………………………………………………………………………………………………………………….**

**UHUSIANO……………………………………………………………………………………………………………………………………………………**

**KAZI YA MZAZI/MLEZI……………………………………………………………………………………………………………………………………**

**KIAPO CHA UTII**

**MIMI (JINA LA MWANAFUNZI)…………………………………………………………..**

Nikiwa mwanafunzi wa shule hii nakubali kuwa ,Uma wa nchi hii ya Tanzania ndio ulionipa nafasi hii maalumu ya masomo,ili nimalizapo niweze kuitumikia nchi yangu kwa nguvu zangu zote na kwa uadilifu .Ninaahidi kwa kipindi chote nitakachokuwa katika shule hii nitakuwa mtiifu ,sitoshiriki katika mgomo ,fujo,wala makosa ya jinai.Nitalinda amani na utulivu wa shule kwa njia zozote ikiwamo kutoa taarifa kwa uongozi wa shule kuhusu jambo lolotelinaloashiria uvunjifu wa amani shuleni.

Ninajua kuwa serikali inatumia raslimali zake nyingi kugharamia elimu yangu na mimi ninaahidi kuwa masuala ya taaluma nitayapa kipaumbele cha kwanza ikiwa ni pamoja na kuwaheshimu

walimu,wafanyakazi wasio walimu na wanafunzi wenzangu wote na kuhudhuria vipindi vyote darasani.

Nikiwa na malalamiko au maoni yeyote nitayafikisha kwa uongozi wa shule kwa kufuata utaratibu uliowekwa

Tarehe………………………………………………………………

Sahihi………………………………………………………………………………………

**KIAPO CHA MZAZI /MLEZI**

Mimi mzazi/mlezi wa (Jina la mwanafunzi)…………………………………………………………………………

Ninakiri kuwa nimesoma,nimeelewa na ninakubaliana na sheria ,kanuni na taratibu zote zilizoainishwa za kujiunga na shule hii,na pale mwanangu atakapozikiuka hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake.

Sahihi…………………………………………………………………………….

Tarehe………………………………………………………………….

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

SEHEMU A

1. JINA(Majina matatu):

| |
|---|
| |

2.Tarehe ya kuzaliwa

3.Utaifa

| | |
|---|---|
| Utaifa: | Mkoa: |
| Wilaya | Kabila: |

4.TAARIFA YA KUBAINI WANAFUNZI YATIMA (WEKA ALAMA YA VEMA PANAPOSTAHILI)

i. Baba na mama wote walikwishafariki ( )
ii. Baba yupo,mama alikwishafariki ( )
iii. Mama yupo,baba alikwishafariki ( )
iv. Baba na mama wote wapo ( )

5.Jina la Baba/Mlezi…………………………………………………………………………………………………

Kazi yake…………………………………………………………………………………………Anwani ya Baba/Mlezi……………………………………………………………………………………………………

Namba ya simu ya Baba/Mlezi……………………………………………………………………………….

Anwani ya anakofanyia kazi…………………………………………………………………………………….

6. Jina la Mama/Mlezi………………………………………………………………………………………

Kazi yake……………………………………………………………………………………Anwani ya Mama/Mlezi…………………………………………………………………………..

Namba ya simu ya Mama/Mlezi…………………………………………………………………………………

Anwani ya anakofanyia kazi……………………………………………………………………………………

Je,wazazi wako wanaishi pamoja?weka alama ya vema panapohusika Ndiyo ( ) Hapana ( )

7. (a)Dini yako……………………………………………………………………….

(b)Dhehebu………………………………………………………………………………

8. Taarifa za maendeleo shuleni zitumwe kwa nani ?

Jina……………………………………………………………………………………………………………………………….

Anwani yake…………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………..

**TAARIFA KUHUSU SHULE ANAYOTOKA MWANAFUNZI**

9.Jina la shule yamsingi uliyosoma……………………………………………………………………………………

Jina la Mwalimu ……………………………………………………………………………………………………………

Anwani ya shule hiyo ni………………………………………………………………………………………………………

Namba ya simu ya mwalimu mkuu wa shule uliyotoka ………………………………………………………

Prem namba…………………………………………………………………………………………………………………

**ORODHA YA NDUGU /JAMAA WA MWANAFUNZI**

Fomu hii ijazwe na kila mzazi wa mwanafunzi akitoa maelezo sahihi ya Ndugu/jamaa zake wane watakaompa motto wake huduma mbalimbali wakati akiwepo hapa shuleni.Watakaoorodheshwa ndio pekee watapata ridhaa ya kushughulikia masuala ya mwanafunzi awapo shuleni hususani yanapotokea matatizo ya kinidhamu na hata kumtembelea.

| S/N | JINA LA NDUGU/JAMAA | MNAVYOHUSIANA | ANWANI YAKE | PICHA YA PASPOTI SIZE YA MZAZI/JAMAA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4 | | | | |

NATHIBITISHA KUWA TAARIFA HII NI SAHIHI:
Sahihi ya mzazi /mlezi………………………………………………………………………………..
Sahihi ya mwanafunzi………………………………………………………………………………..
Tarehe………………………………………………………………………………………………………….

**SONGWE TECHNICAL SECONDARY SCHOOL MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by a Medical Officer (Government hospital)

NAME……………………………………………………………………………………………………….FORM………..

BLOOD COUNT

(Red and White)……………………………………………………………………………………………….……………

STOOL EXAMINATION…………………………………………………………………………………………….……

URINE ANALYSIS………………………………………………………………………………………………………………..

SYPHILIS TEST…………………………………………………………………………………………………………..………

T.B.TEST………………………………………………………………………………………………………………………………

EYE TEST…………………………………………………………………………………………………………..…………

EARS………………………………………………………………………………………………………………………………….

SPLEEN……………………………………………………………………………………………………………………………..

ABDOMEN………………………………………………………………………………………………………………….

PREGNANCY TEST………………………………………………………………………………………………………………

ADDITIONAL information e.g Physical defects or

impairments…………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………

Infections,chronic or family diseases

etc…………………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………………

Please certify that the above is fit to be enrolled at Songwe Technical secondary school

Signature……………………………………………………………………………..

Designation………………………………………………………………………………

Station……………………………………………………………………………………….

Date…………………………………………………………………………………………..